ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority

# Newsletter

OKTOBA 2012

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 007

# FCT yatupilia mbali rufani ya Kampuni za mafuta kupinga kanuni mpya ya bei



# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Waraka wa Mhariri | pg-3 |
| Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu | pg-4 |
| FCT yatupilia mbali rufani ya Kampuni za mafuta kupinga kanuni mpya ya bei | pg-5 |
| Masebu kuongoza wadhibiti barani Afrika | pg-7 |
| Bei ya mafuta Tanzania huenda ni nafuu kuliko nchi jirani- EWURA | pg-8 |
| Tanzania kuwa kituo cha  wa uzalishaji wa gesi asili | pg-9 |
| Ewura yaongeza pato la taifa kupitia mradi wa uwekaji vinasaba  kwenye mafuta | pg-11 |
| Juhudi za usambazaji umeme vijijini: Mwenga Hydro Limited yaonesha njia | pg-13 |
| Mbinga kupata umeme wa maji wa *Megawati* 7.5 | pg-14 |
| Matukio katika picha | pg-16 |
| | pg-19 |






## BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Mr. Haruna Masebu

**MHARIRI**
Mr. Titus Kaguo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Mr. Wilfred Mwakalosi

**WAJUMBE**
Ms. Miriam G. Mahanyu
Mr. Felix Ngamlagosi
Eng. Charles S. Omujuni

**SEKRETARIETI**
Ms. Hawa Lweno
Ms. Janet Mwaipopo



**OFISI YA EWURA**
Ghorofa ya Sita, Habour View
Towers, Barabara ya Samora
S. L. P. 72175,
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 - (22) 2123850/3/4/6
Nukushi: +255 - (22) 2123180
B/Pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: www.ewura.go.tz

# Waraka wa Mhariri



**Bw. Titus Kaguo**

KARIBU katika toleo la Jarida letu tulipendalo la Mamlaka ya udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Toleo hili ni kati ya matoleo mengi ambayo yameshachapishwa, yakiwa na lengo, pamoja na mambo mengine, kutekeleza maagizo ya Sheria ya EWURA, Sura namba 414 ya Sheria za Tanzania.

Ibara ya 6 (e) ya Sura namba 414 inaipa Mamlaka wajibu wa uelimisha umma juu ya sekta zinazodhibitiwa kuhusu wajibu na haki kwa watoaji na watumiaji huduma; jinsi ya kuwasilisha malalamiko na kutatua migogoro, wajibu, majukumu na shughuli za Mamlaka.

Likiwa ni toleo la Saba, Jarida la EWURA limekuwa ni nyenzo mahususi ya kufikisha ujumbe kwa umma, hivyo kuwafanya watoa huduma na watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA kuwa na ufahamu mkubwa juu ya haki na wajibu wao.

Tangu tulipoanzisha Jarida la EWURA, ambalo linasomeka kiurahisi kwa wanaotumia Lugha za Kiswahili na Kiingereza, Mamlaka imeshuhudia kuongezeka kwa ufahamu juu ya wajibu wetu katika sekta ndogo nne zinazodhibitiwa za Petroli, Umeme, Ges Asili na Maji.

Katika toleo hili, wasomaji wataendelea ufurahia makala mbalimbali kama vile hukumu ya kesi iliyofunguliwa na Kampuni za mafuta dhidi ya EWURA kupinga kanuni mpya ya bei, mchango wa uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta, jinsi Tanzania itakavyokuwa eneo kuu la masuala ya gesi asili na habari nyingi nyingi.

Pia, ni matarajio yetu kuwa, wasomaji watafahamu jinsi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Bw. Haruna Masebu, alivyochaguliwa kushika nafasi ya juu kabisa ya uongozi barani Afrika katika sekta ya udhibiti.

Karibu ufurahie jarida letu!

# Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu



**Bw. Haruna Masebu**

Wapendwa wasomaji wa toleo la saba la jarida la EWURA, ni furaha yangu kwa mara nyingine tena kuwakaribisha kusoma na kufurahia makala zinazohusu masuala ya sekta za Umeme, Mafuta, Gesi Asilia na Maji.

Kwa kipindi kifupi kilichopita, EWURA imekuwa ikizingatia maeneo mawili yenye maslahi ya uchumi wa taifa. Maeneo haya ni kuendelea kutekelezwa kwa mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja, yaani Bulk Procurement System (BPS) na kukamilika kwa utafiti wa gharama halisi za umeme yaani Cost of Service Study (COSS).

Ndugu msomaji, kama mjuavyo, mfumo wa BPS ulizinduliwa mnamo Januari 2012, ambapo shehena ya kwanza ya mafuta ya petroli kutumia mfumo wa BPS iliwasili nchini. Tangu wakati huo, kampuni ya Petroleum Importation Coordinator (PIC) imekuwa na mafanikio makubwa katika uratibu wa mchakato wa zabuni za uagizaji wa bidhaa za mafuta, ambapo kampuni ya Augusta Energy ndiyo iliyokuwa mshindi wa zabuni tatu kwa mfululizo.

Mnamo Agosti 2012, kampuni ya Addax ilishinda zabuni ya nne chini ya mfumo wa BPS ikiwa ni ishara ya hali ya ushindani mkali wa zabuni zilizopo chini ya mfumo huo. Hivyo, mfumo wa BPS unaendelea kuonyesha kwamba umefanya kazi vizuri na kwa mafanikio makubwa! BPS pia imeonyesha faida kubwa kwa nchi kutokana na ongezeko la mapato ya kodi zilizokusanywa na Serikali kwenye kipindi Januari-Agosti 2012. Hata hivyo, changamoto bado ni nyingi kwenye mfumo huu mpya. EWURA itaendelea kushirikisha wadau wote ili kuhakikisha kwamba maoni yote yanashughulikiwa na kupewa kipaumbele kwa ajili ya kuboresha mfumo wa BPS.

Katika sekta ya umeme, EWURA ilikabiliwa na changamoto kubwa kutokana na hali ya ukame iliyosababisha kuongezeka kwa utumiaji wa mitambo ya dharura na baadae kusababisha ongezeko la bei ya umeme kwa asilimia 40.29 badala ya ongezeko la asilimia 155 iliyoombwa. Kutokana na mwelekeo huu, EWURA iliamua kufanya Cost of Service Study (COSS) kwa lengo la kupata tathmini sahihi ya gharama za kufanya biashara kutoka TANESCO. Pamoja na utafiti huu, Mshauri, PF Mercados wa Hispania, alipewa kazi ya kutoa mapendekezo iwapo bei ya umeme ni sahihi kutokana na gharama halisi ya kuzalisha umeme. Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na mshauri, EWURA ina furaha kwamba tayari kazi hiyo imeshafanyika na taarifa husika zimepokelewa na Mamlaka, na hatimaye kupelekwa kwa wadau wote kwa lengo la kukusanya maoni yatakayozingatiwa na mshauri katika ripoti ya mwisho.

Ni muhimu kutambua kuwa matokeo ya taarifa hizi za utafiti yanatarajiwa kutumika na Mamlaka katika utoaji wa uamuzi wa mwisho juu ya ombi la TANESCO la kupitia bei ya umeme kama mojawapo ya hatua za dharura dhidi ya uhaba wa umeme nchini. Uamuzi wa Mamlaka juu ya maombi ya TANESCO inatarajiwa kutangazwa Oktoba 2012.

Mpendwa msomaji, kama mamlaka ya udhibiti katika sekta za Umeme, Gesi Asilia, Mafuta na Maji, EWURA itaendelea kuzingatia viwango vya kimataifa katika udhibiti wa sekta hizi hivyo kuhakikisha kuwepo kwa soko lenye haki na ushindani kwa washiriki wote. Kwa kufanya hivyo, EWURA itaendelea kutambulika kama mamlaka ya udhibiti mashahuri hapa Tanzania na barani Afrika. Katika suala hili, EWURA ina furahi kuwa Mkurugenzi wake Mkuu ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa African Forum for Utility Regulators (AFUR), kwa kipindi cha miaka mitatu baada ya kupigiwa kura na wanachama wa AFUR katika mkutano wao mkuu uliofanyika Machi 2012.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za mamlaka.

Tafadhali ungana na mimi katika kusoma makala zinazopatikana katika jarida hili la EWURA.

# FCT yatupilia mbali rufani ya Kampuni za mafuta kupinga kanuni mpya ya bei

**Na Mwandishi wetu**



BARAZA la Rufani la Ushindani wa Haki za Kibiashara (FCT), limetupilia mbali rufaa iliyofunguliwa na Kampuni 13 dhidi ya Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishatji na Maji (EWURA), kutaka Baraza hilo kubatilisha mfumo wa ukokotoaji wa bei za mafuta uliyofanikisha kushuka kwa bei mwaka 2011.

Kampuni zilizokata rufaa hiyo ni pamoja na BP Tanzania, (sasa Puma Tanzania Ltd), Total (T) Ltd, Gapco (T) Ltd, Hass Petroleum (T) Ltd, Oryx Oil Company Ltd, MGS International (T) Ltd, GBP (T) Ltd, Lake Oil Ltd, MOIL (T) Ltd, Engen Petroleum Tanzania Ltd, Camel Oil (T) Ltd, Oilcom (T) Ltd na ACER Petroleum (T) Ltd.

Kampuni hizo pia zilikata rufaa dhidi ya Agizo la EWURA kwa Kampuni nne za BP Tanzania , Engen Petroleum Tanzania Ltd, Camel Oil (T) Ltd and Oilcom (T) Ltd, la kuzitaka kampuni hizo zianze kuuza mafuta mara moja.

Katika uamuzi wake, Baraza hilo chini ya Mwenyekiti wake Jaji Razia Sheikh, liliamua kuwa rufani hiyo haikuwa na mashiko na hivyo kutupiliwa mbali huku Kampuni hizo zikitakiwa kulipa gharama zote za shauri hilo.

Hukumu hiyo inamaliza msuguano wa kisheria uliodumu kwa muda wa mwaka mmoja kati ya Kampuni za Mafuta na Mdhibiti, juu ya njia mpya ya kukokotolea bei za mafuta, hali iliyofanya kuadimika kwa mafuta nchini mara bei hizo zilipotangazwa mwezi Agosti mwaka 2011.

Pamoja na mambo mengine, Kanuni hiyo ya kukokotolea bei za mafuta iliondoa wigo wa faida wa asimilia 7.5 ambayo wafanyabiasahara walikuwa wakifaidika nayo tangu kuwekwa mwaka 2009, ikilenga kufidia baadhi ya matatizo ya kibiashara.

Pia Kanuni hiyo ilipunguza gharama ya upotevu wa mafuta baharini kutoka asilimia 0.5% kwa mafuta ya petroli hadi 0.25, na kutoka asilimia 0.30 kwa dizeli na mafuta ya taa hadi 0.15 ya gharama, bima na thamani ya usafirishaji.

Walalamikaji waliowakilishwa na Kampuni ya Uwakili ya IMMA, walilalamika kuwa EWURA ilikosea kisheria kwa kushindwa kuoanisha gharama na faida za biashara hiyo katika nyanja za kimataifa.

"Mlalamikiwa (EWURA) alikosea kisheria hususan kutoa kanuni ya kukokotolea bei iliyo chini hivyo kutoruhusu ushindani baina la walalamikaji, hiyo kuwafanya kuweka bei yenye mwelekeo wa kupanga," inasema sehemu ya rufani hiyo.

Walalamikaji pia waliilaumu EWURA kushindwa kuzingatia kigezo cha maslahi ya mwekezaji na mlaji wa huduma; EWURA ilishindwa kulinda mitaji ya walalamikaji na ilishindwa pia kuchochea mazingira mazuri ya ushindani na uchumi.

"Mlalamikiwa alikiuka sheria kwa mlalamikaji wa kwanza, pili, tatu na wa nne kwa kutoa agizo la kuuza mafuta ya petroli kwa hasara," walidai walalamikaji.

Kwa ujumla kampuni za mafuta zilidai kuwa uamuzi wa EWURA ulikiuka kazi na wajibu wake chini ya Sheria ya EWURA na kwamba kanuni ya kukokotoa bei ilifikiwa kutokana na msukumo wa kisiasa.

Ikiwakilishwa na Kampuni ya Uwakili ya GRK, huku ikiongozwa na Bw. Zephrine Galeba, EWURA ilijibu tuhuma hizo kuwa si za kweli kwa kuwa kanuni ya kukokotolea bei za mafuta ilifikiwa kwa kuzingatia maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wakiwamo walalamikaji na umma.

"...katika kufikia kanuni ya kukokotolea bei za mafuta, mlalamikiwa alitekeleza vipengele vyote vya kisheria na zaidi mlalamikiwa alihaikisha masuala yote yanayotakiwa katika mchakato wa kutengeneza kanuni ya kukokotoa bei yanajadiliwa wakati wa taftishi," EWURA ilijibu.

Kuhusu Agizo, mlalamikiwa (EWURA) alisema yeye hakuamuru kampuni za mafuta kuuza mafuta kwa hasara.

"EWURA ilichokifanya ni kuagiza Kampuni nne kuacha kutouza mafuta, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria kwa kutouza au kusambaza mafuta kwa mujibu wa bei kikomo," aliongeza Mwanasheria wa EWURA.

Likitoa hukumu, Baraza lilisema mlalamikiwa alikuwa amefanya kazi yake vizuri kama mdhibiti alipokuwa akitengeneza kanuni ya kukokotolea bei za mafuta.

" Suala kuhusu mtengamano wa kifedha halina mashiko, linapotosha na linakwepesha ukweli kwa kuwa mlalamikaji hakuonesha jinsi mlalamikiwa alivyopaswa kufanya kuhakikisha suala hilo linaingizwa kwenye mchakato," linasema Bazara.

Baraza lilisema kuwa katika kufikia kwenye Kanuni mpya, mlalamikaji aliviangalia vipengele vikiwamo maslahi ya walaji na wawekezaji, gharama za kusambaza bidhaa za petroli na masuala mengine yaliyowekwa na Sheria ya EWURA kifungu cha 6 na 17.

"Katika mazingira haya, kwa sababu zilizopo hapo juu, tunaridhika kuwa malalamikiwa hakukiuka kutoa agizo, kwa kuwa haipingwi kuwa walalamikaji wanne walikataa kufanya biashara na hivyo kwenda kinyume na uamuzi wa EWURA," Baraza liliamua.

Kanuni mpya pia ilipunguza gharama za uwekezaji kutoka asilimia 1.75 ya thamani ya gharama ya uagizaji mafuta (CFI) hadi asilimia 0.25 na kuanza kutumia ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa kuzingatia viwango vya Banki Kuu ya Tanzania.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Bw. Titus Kaguo, akizungumzia hukumu hiyo, alisema EWURA imefurahiswa sana kwa kuwa uamuzi huo umeonyesha umma kuwa uamuzi wa EWURA huwa si wa kukurupuka, bali unafuata sheria na vigezo vya kitaalam.



Ushirikishwaji: Moja ya njia bora za Mdhibiti kufanya kazi zake kwa uwazi ni kuruhusu wadau kushiriki kikamilifu kama inavyoonekana pichani, ambapo wadau wa sekta ndogo ya petroli wakiwa kwenye moja ya mikutano iliyoitishwa na EWURA, jijini Dar es Salaam.

# Masebu kuongoza wadhibiti barani Afrika

Hatua hii imekuja, baada ya mwaka 2010, Bw. Masebu kuchaguliwa kuwa Kiongozi bora wa mwaka, ambapo aliibuka mshindi miongoni mwa Wakurugenzi wakuu wa mashirika 18 hapa nchini.

**Na Mwandishi Wetu**



**Bw. Haruna Masebu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Bw. Haruna Masebu, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadhibiti wa Huduma Barani Africa (AFUR).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Meneja wa Idara ya Mawasiliano na Uhusino wa EWURA, Bw. Titus Kaguo, uchaguzi huo ulifanyika hivi karibuni jijini Pretoria, Afrika Kusini.

Bw. Kaguo alisema jina la Bw. Masebu kugombea Uenyekiti huo lilipendekezwa katika Mkutano wa tisa wa Mwaka wa AFUR na ujumbe wa Mdhibiti wa Umeme wa Cameroun ambapo, ilikubaliwa na wajumbe wengine zaidi ya 20. Tofauti na chaguzi za wenyeviti wengine wawili waliopita akiwamo aliyeondoka madarakani, Profesa Asie Benne kutoka Ivory Coast, ambao walikuwa wakipigiwa kura ya siri, Bw. Masebu alichaguliwa kwa kura za wazi na wajumbe zaidi ya 20.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Bw. Masebu ambaye katika mkutano huo aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA, Bw. Simon Sayore, alisema kuchaguliwa bila kupingwa, huku akiwa mgombea pekee tofauti na uchaguzi uliopita, ni ishara tosha kuwa Jukwaa limemwamini kwa utendaji wake na limempa nguvu ya kuliongoza kwenye viwango vya juu.

"Tunapojenga Jukwaa hili la Wadhibiti, kila mmoja wetu anatakiwa kuwajibika ili kuendeleza maadili tuliyojiwekea wakati tukiendelea kuiboresha taasisi hii," alisema Masebu na kuongeza: " Tunachokihitaji zaidi ni ushirikiano, kubadilishana mawazo na kujifunza baina yetu kwa manufaa ya nchi zetu na Bara la Afrika kwa ujumla."

Hatua hii imekuja, baada ya mwaka 2010, Bw. Masebu kuchaguliwa kuwa Kiongozi bora wa mwaka, ambapo aliibuka mshindi miongoni mwa Wakurugenzi wakuu wa mashirika 18 hapa nchini.

AFUR ilianzishwa Novemba mwaka 2002 kama chama cha wadhibiti wa huduma barani Afrika, makao yake makuu yakiwa Pretoria, Afrika ya Kusini.

Madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kuongeza na kuupa nguvu ushirikiano baina ya wadhibiti wa huduma barani Afrika katika jitihada za kukuza uchumi na mifumo ya kijamii kwa wananchama.

AFUR imejikita katika masuala kama ya Nishati, Mawasiliano, Usafirishaji na Maji Safi na Maji Taka. Pamoja na mambo mengine mpango na maono ya AFUR ni kuweka mifumo thabiti ya udhibiti ulioimara baina ya wanachama katika kuleta maendeleo ya miundombinu na huduma barani Afrika. AFUR inawanachama zaidi ya 30 kutoka katika nchi 20 barani Afrika.
other countries.

# Bei ya mafuta Tanzania huenda ni nafuu kuliko nchi jirani- EWURA

Kama isingelikuwa mfumo huu, bei za kwenye vituo zingeongezeka kwa asilimia tano zaidi kufanya asilimia 9...tumeweza kupunguza hii kwa kudhibiti idadi ya meli zinazoleta shehena ya mafuta

**Na Wilfred Mwakalosi**

Licha ya kuwa bei za jumla na reja reja za bidhaa zote za petroli katika soko la ndani Tanzania Bara zimekuwa zikipanda hivi karibuni, bei hizo ni matokeo ya mabadiliko kwenye soko la dunia, ambapo bei za bidhaa hizo zimekuwa zikipanda.

Bei za rejareja mwanzoni mwa mwezi Mei ziliongezeka, ambapo petroli ilifikia TZS 87 au asilimia 4.06, dizeli TZS 3 au asilimia 0.14 na mafuta ya taa TZS 12 au asilimia 0.59. Sababu kubwa ya mabadiliko hayo ilikuwa ni mabadiliko kwenye soko la dunia, ambako petroli ilipanda kwa wastani wa dola za Kimarekani 95.7 kwa tani au asilimia 9.09, dizeli kwa dola 27.1 kwa tani au asilimia 2.76 na mafuta ya taa dola 34.04 kwa tani au asilimia 3.28.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA Bw. Titus Kaguo, amesema kuwa hata hivyo, bei za mafuta zinaziathiri nchi nyingi barani Afrika na duniani kote kwa ujumla, na kwamba EWURA imekuwa ikifanya jitihada za dhati kuhakikisha kuwa kama kuna ulazima wa mafuta kubadilika bei, basi itakuwa hivyo kwa sababu halisi tu na kwa kuzingatia hali ya soko la dunia ili kuepuka udanganyifu.

"Ukifanya mlinganisho, mafuta yauzwayo Tanzania ni ama rahisi ukilinganisha na nchi jirani katika Afrika Mashariki, au bei zinawiana na za nchi nyingine, kinyume na imani ya baadhi yetu kuwa nchi kadhaa, zikiwemo zinazotumia bandari yetu, zinauza mafuta kwa bei rahisi kuliko Tanzania," alisema.

"Ukifanya mlinganisho, mafuta yauzwayo Tanzania ni ama rahisi ukilinganisha na nchi jirani katika Afrika Mashariki, au bei zinawiana na za nchi nyingine, kinyume na imani ya baadhi yetu kuwa nchi kadhaa, zikiwemo zinazotumia bandari yetu, zinauza mafuta kwa bei rahisi kuliko Tanzania," alisema.

Bw. Kaguo alisema, kwa mfano, mwezi Mei katika mabadiliko ya bei za mafuta, Kenya ambayo ina kiwanda cha kusafisha mafuta ilitangaza bei kikomo kwa petroli KSH 118.50 (TZS 2,255.78), na dizeli KSH 108.80 (TZS 2071.13) mjini Nairobi. Nchini Uganda, petroli kwa mwezi huo huo iliuzwa kwa wastani wa dola za Kimarekani 1.70 (TZS 2,686.00), dizeli iliuzwa dola ya Kimarekani 1.34 (TZS 2,117.20), wakati Malawi petroli iliuzwa dola 2.05 (TZS 3,239.00), dizeli dola 1.85 (TZS 2,923.00).

Zambia, nchi nyingine yenye kiwanda cha kusafisha mafuta na inayotumia sana bandari ya Dar es Salaam, mwezi Mei ilikuwa inauza petroli kwa dola za Kimarekani 1.82 (TZS. 2,875.00) na dizeli dola 1.40 (TZS 2,212.00), wakati Burundi, nchi isiyo na bandari, na hivyo hutumia ya Dar es Salaam, iliuza petroli kwa wastani wa dola 1.72 (TZS 2,717.60) na dizeli dola 1.7 (TZS 2,686.00). Rwanda, ambayo kama Burundi haina bandari, iliuza petroli kwa wastani wa dola

1.96 (TZS. 3,096.80) na dizeli dola 1.95 (TZS 3,081.00). Bwana Kaguo alisema hata hivyo, Angola moja ya nchi zinazozalisha mafuta barani Afrika ilikuwa inauza petroli kwa wastani wa dola 0.78 (TZS 1,232.00) na dizeli dola 0.52 (TZS 821.60), wakati Ghana ilikuwa inauza petroli kwa dola 0.99 (TZS.1,564.20.) na dizeli dola 1.00 (TZS. 1,580.00) —ikiwa bei ya chini kuliko Tanzania.

Hata hivyo Bw. Kaguo amesema bei za mafuta katika soko la dunia huchangia kwa asilimia ...kwenye bei za vituoni hapa nchini, na kwamba kodi za serikali huchangia kwa asilimia .... wakati tozo za kiudhibiti zinachangia kwa asilimia....

Kuhusu kwa nini bei za mafuta hazionekani kushuka, kinyume na matarajio ya wengi kwamba mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja ungesababisha unafuu wa bei kwa mtumiaji wa mwisho, Bw. Kaguo amesema bei ni sehemu ndogo sana ya faida ya mfumo huo wa uagizaji wa pamoja.

"Kama isingelikuwa mfumo huu, bei za kwenye vituo zingeongezeka kwa asilimia tano zaidi kufanya asilimia 9...tumeweza kupunguza hii kwa kudhibiti idadi ya meli zinazoleta shehena ya mafuta, hivyo kuokoa tozo za ucheleweshaji meli bandarini ambazo hulipishwa mlaji wa mwisho," alisema, na kuongeza kwamba mambo mengine kama kudhoofu kwa sarafu ya shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani, gharama za kusafirisha shehena pamoja na gharama za bima, ni vigezo vikubwa katika kufikia bei za mafuta.

Hata hivyo, alisema EWURA inauona mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kama wenye tija na manufaa ambayo yataonekana hivi karibuni, hasa miundombinu ya kupakulia mafuta bandarini itakapoongezwa na kuboreshwa ili kuweza kupokea meli kubwa zaidi.

# Tanzania kuwa Kituo cha uzalishaji wa gesi asili

Kundi la makampuni la BG, Petrobas na Statoil zimegundua kuwepo kwa gesi katika pwani ya Tanzania, ambayo inakadiriwa kuwa futi za ujazo trilioni 10.

**Na Mhandisi Thobias Rwelamila**

Wakati fulani ikishindwa kuvutia kampuni za kimataifa ya mafuta na gesi, Tanzania sasa inatazamia kuwa nchi inayozalisha gesi kwa wingi Afrika Mashariki, kufuatia ugunduzi wa bidhaa hiyo.

Kundi la makampuni la BG, Petrobas na Statoil zimegundua kuwepo kwa gesi katika pwani ya Tanzania, ambayo inakadiriwa kuwa futi za ujazo trilioni 10. Inategemewa kwamba ugunduzi wa gesi kwa kampuni hizi tatu utaongeza kiwango cha gesi asilia kilichopo nchini ambacho sasa kinafikia futi za ujazo trilioni 1.5.

Ugunduzi kama huu wa gesi asilia nchini ni nafasi ya kipekee kiuchumi, lakini pia ni hatari kwa nchi. Gesi asilia, na hasa hasa mafuta vinaweza kuwa msaada mkubwa wa kusisimua ukuaji wa uchumi ama vinaweza kutibua maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambayo Taifa imepata.

Hata hivyo, changamoto kubwa mbele yetu kama taifa ni namna gani Tanzania itaweza kutumia hazina yake ya gesi asilia kwa kigeuza kuwa mtaji wa maendeleo ya rasilimali watu na jamii kwa ujumla, kupitia uwekezaji—vinginevyo nchi itapoteza utajiri wake huu siku zijazo.

Nchi nyingine kama Nigeria ambazo zimejaliwa raslimali kama hizi, changamoto hizi si ndogo kwa sababu nchi nyingi zinazotegemea gesi na mafuta zimekuwa zikifuja utajiri huu kwa muda mrefu bila kupatikana kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kwa kuzingatia ugunduzi huu wa gesi, kuna umuhimu wa kutafuta namna ya kuongeza mahitaji ya soko la ndani kwa kuanza kutayarisha mtazamo wa viwanda vitakavyoweza kutumia gesi. Tunahitaji kuchochea uwekezaji wa ndani na nje wa viwanda vitakavyotumia gesi kutengeneza mbolea kama Ammonia au Urea ili kuweza kuteka soko la kimataifa la mbolea na bidhaa za petrli na kemikali.

**Muundo wa sasa wa soko la ndani**

Gesi inayozalishwa Songo Songo inatumiwa kuzalisha umeme (kwa sasa futi za ujazo milioni 90) na inatumika kama nishati kwenye kiwanda cha kutengeneza sementi na nishati mbadala kwenye kampuni ya Sigara (TCC) na kiwanda cha nguo cha Urafiki.

Viwanda 36 jijini Dar es Salaam sasa vimeunganishwa kwenye bomba la gesi na vinatumia gesi hiyo kwa ajili ya mifumo ya uchemshaji na uchomaji. Hivi karibuni, yameanza matumizi ya Gesi Asilia kwenye magari na makazi. Matumizi ya viwanda ni jumla ya futi za ujazo milioni 10 kwa siku, lakini kutokana na mahitaji kidogo ya umeme kwa mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara, ni futi za ujazo milioni moja tu kwa siku zinatumika kuzalisha umeme wa karibu Megawati 11.
Soko la gesi kwa ajili ya viwanda jijini Dar es Salaam limefikia ukomo wake, lakini inategemewa kwamba soko litaendelea kukua kutegemea maendeleo ya kiuchumi na upatikanaji wa umeme. Soko la gesi ya kuendeshea magari bado lina nafasi ya kupanuka.

Uwepo wa soko la bidhaa za kikemikali na bidhaa nyingine zinazotegemea gesi au mafuta haujafanyiwa utafiti wa kutosha bado. Miaka ya nyuma, wawekezaji wengi walionesha nia yao ya kutaka kuwekeza kwenye uzalishaji wa methanol na mbolea.

Mahitaji ya nishati ya umeme yanategemewa kuongezeka kwa kati ya asilimia 10 na 15 kwa mwaka, jambo ambalo litachangia kukua kwa mahitaji ya gesi. Ongezeko hili limechochea kuanzishwa kwa miradi mingi, ikiwa ni pamoja na ule wa megawati 340 wa gesi kufua umeme ambao unatarajiwa kukamilika 2012, na upanuzi wa mtandao wa kusambaza umeme unaotarajiwa kukamilika mwaka 2015.

Kampuni ya Utafiti na Uzalishaji ya Orca, ambayo kupitia kampuni yake tanzu PanAfrican Energy inaendesha mradi wa Songo Songo, ina mpango wa kuongeza uzalishaji kwa asilimia 60 kufikia futi za ujazo 144 kwa siku.

Hatua hii inahitaji upanuzi wa bomba lililopo na uwezo wa uchakataji. Lakini mahitaji ya ndani ya gesi, licha ya makisio ya ukuaji wa mahitaji hayo, yataweza kufikia robo tu ya hazina yote iliyogunduliwa, vinginevyo jitihada za pamoja zifanywe kuongeza mahitaji ya soko la ndani kupitia uzalidhaji nishati na matumizi ya viwandani. Kushindwa kwa soko la ndani kutumia gesi yote asilia kutazilazimisha kampuni zinazogusika kutafuta masoko ya nje ya nchi ili kupata fedha za kuendeleza utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia.

**Uuzaji wa Gesi nchi za nje**

Uuzaji wa kwenye masoko ya kikanda kama Afrika Mashariki utahitaji upanuzi wa mitambo ya kuchakata gesi na ufungaji wa mitambo ya kusukumia gesi kwenye bomba la Songas ili kuongeza uwezo wake. Vinginevyo, ujenzi wa bomba jipya utahitajika, pamoja na uwezekano wa kurefusha bomba hilo zaidi ya Dar es Salaam, ili kuwapa nafasi wanunuzi wengine. Mara hifadhi hiyo ya gesi itakapoonekana kuwa imekuwa 'kubwa sana,' makampuni ya kimataifa ya mafuta yatatafuta namna ya kuiuza gesi hiyo kwenye soko la kimataifa, ambako watapata faida kubwa. Jambo ambalo watunga sera na taasisi

za serikali wanapaswa kulizingatia ni kwamba makampuni mengi ya mafuta ya kimataifa yenye hifadhi zaidi ya futi trilioni tatu za ujazo gesi asilia (LNG), inawezekana yaona gesi hii ikawa chaguo sahihi kwa ajili ya soko la kimataifa.

Licha ya ugunduzi wa hifadhi kubwa kiasi hiki, serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba haijifungi kuuza nje ya nchi gesi hii kwa siku zijazo, kwa sababu kuna hatari ya kuishiwa gesi kwa ajili ya matumizi ya nchini, kama ilivyo kwa Misri.

Ingawa si yenye faida kubwa ukilinganisha na kusafirisha gesi nje ya nchi kwa bomba, miradi ya urea au amonia na methano inaweza kuanzishwa pale ambapo gesi inapatikana kwa kiwango kidogo, au pale ambapo mtaji ni mdogo, jambo ambalo linaweza kuwa linaikabili Tanzania.

Kijiografia, Tanzania ni nchi ambayo imekaa kimkakati kuweza kuuza mbole kwenye nchi watumiaji wakubwa ikiwa ni pamoja na Asia Kusini, Afrika Kaskazini, na Asia Mashariki. Methano, ambayo hutumika katika uzalishaji wa kemikali zenye asili ya petroli, inaweza kufanyiwa utafiti sambamba na urea na amonia au ikiwa peke yake.

Wakati masoko ya kiasili ya kemikali zenye asili ya petroli Afrika Kaskazini na Ulaya Magharibi kwa sasa hayajachangamka, kuna mahitaji makubwa China na nchi nyingine za Kiasia. Huku hifadhi zaidi zikigunduliwa, yafaa kama nchi kuangalia ni kwa namna gani bidhaa hii inaweza kuuzwa kwenye masoko hayo ili kuwezesha makampuni ya kimataifa ya mafuta kupata fedha za kuzalisha gesi asilia na hatimaye kuifanya Tanzania kituo kikuu cha gesi asilia katika Afrika Mashariki.




Mkurugenzi wa Bodi ya EWURA, Bw. Nicholaus Mbwanji (wa pili toka kushoto), Mkurugenzi wa EWURA wa Gesi Asilia, Mhandisi Charles Omujuni, (wa tatu kulia) na Meneja wa EWURA wa Usambazaji wa Gesi Asilia, Mhandisi Thobias Rwelamila (kulia) wakikagua miundombinu ya gesi kwenye kiwanda cha Sigara Tanzania mwaka 2011. Kushoto ni mwenyeji wao.

# Ewura yaongeza pato la taifa kupitia mradi wa uwekaji vinasaba kwenye mafuta

**Na Mwandishi wetu**



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt. Parseko Ole Kone (wa tatu toka kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Petroli wa EWURA, Mhandisi Julius Gashaza (aliyenyoosha mkono) kuhusu namna mtambo wa kuchunguza ubora wa mafuta wa XRF unavyofanya kazi, wakati wa maonesho ya Nane Nane mkoani Dodoma, Agosti 2012.

WAKATI Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inaanza kuratibu biashara katika sekta ya mafuta nchini mwaka 2006, uchakachuaji mafuta ulikuwa katika kiwango cha juu.

Meneja wa Idara ya Mawasiliano na Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, anasema utumiaji wa mafuta hayo, ulisababisha vyombo vya usafiri kuzalisha hewa chafu yenye sumu, pamoja na kuikosesha serikali kodi ya takribani Sh bilioni 300 kwa mwaka.

Kwa msisitizo, Ewura imeanzisha teknolojia inayotumia kemikali isiyoonekana, iliyopewa jina la "DNA" ambayo kwa muda mfupi imedhibiti ukwepaji kodi na kuongeza matumizi ya mafuta bora.

Katika kukamilisha hilo, Ewura imeingia mkataba na Kampuni ya Global Fluids International (T) Ltd (GFI), ambapo kampuni hiyo imeingiza nchini ving'amuzi maalumu maarufu kama 'vinasaba' vinavyotumia teknolojia ya X-ray Flurescence (XRF) kubaini mafuta yaliyochakachuliwa na kudhibiti kodi. Mashine hizi zimeanza kutumika Septemba 1, 2010.

Takwimu zinaonesha kuwa kwa kutumia mashine hizo, asilimia ya mafuta yaliyokuwa yakikwepa kodi, na sasa yanalipiwa kodi imeongezeka. Kabla ya kutumia mashine hizo kwenye petroli, lita 34, 589, 906 zililipiwa kodi. Mara baada ya kuanza upimaji, katika kipindi cha mwezi mmoja lita 44,010,360 zililipiwa kodi, sawa na ongezeko la asilimia 27.

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi hicho, ukusanyaji wa kodi ya serikali umeongezeka kwa Sh 5,078,702,706, ongezeko ambalo ni sawa na wastani wa Sh 60, 944,432,472 kwa mwaka.

Kwenye dizeli, kabla ya matumizi ya mashine hizo lita 69, 221,971.73 zililipiwa kodi na mara mashine ilipoanza kutumika, lita 87, 065,810 zililipiwa kodi, sawa na ongezeko la asilimia 26.

Ongezeko la malipo ya kodi kwenye dizeli ni Sh 9, 171, 732,732 kwa mwezi, sawa na Sh 110, 061,000,000 kwa mwaka.

Kwenye mafuta ya taa, takwimu zinaonesha kuwa kabla ya upimaji lita 30,025,977.11 zililipiwa kodi, mashine zilipoanza kutumika, lita 19,005,580 zilizipiwa kodi na zikapungua hadi 11,020,397, sawa na asilimia 37.

Kupungua huko kunatokana na kupunguza uagizaji wake, kwani ndio mafuta yaliyotumika sana kuchakachua dizeli. Uagizaji ulipungua baada ya kodi yake kuwa karibu sawa na dizeli, kukomesha uchakachuaji.

Matumizi ya mashine hizo, kumeifanya Ewura ifanye ukaguzi wa mara kwa mara, ambao umeongeza kodi ya serikali kwa wastani wa asilimia 50 kutokana na kuwadhibiti wakwepa kodi.

**Kuanzishwa kwa upimaji wa mafuta kutumia XRF**

Mashine za XRF za kupima mafuta ziliingizwa nchini Septemba mosi 2010, kwa lengo la kudhibiti biashara ya uchakachuaji petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Mashine hizi zinapima mafuta yaliyopakiwa kwenye matangi kutoka kwenye vituo vya kupakilia kwa lengo la kuondoa uchakachuaji, tatizo lililosumbua kwa miaka mingi. Uchakachuaji ulifanywa na wafanyabiashara wanaotaka faida kubwa kwa kuchanganya matufa ya taa kwenye dizeli au petroli wakati bei ya mafuta ya taa ilikuwa ndogo kwa kuwa ilitozwa kodi kidogo.

Uchanganyaji huo, ulisababisha uharibifu afya za watu, mazingira, magari, ukwepaji kodi na kuleta ushindani usio sawa. Tatizo hilo lilivuka nje ya mipaka ya nchi hadi katika nchi jirani, zinazosafirisha mafuta kupitia nchini. Upimaji huo umepunguza wizi kwenye shehena ambayo haijalipiwa kodi inayoingizwa nchini kupitia mipaka isiyoruhusiwa kisheria. Shehena hiyo inaweza pia kuwa mafuta yaliyochakachuliwa nje ya nchi.

Mashine za XRF, haziangalii mafuta yasiyolipiwa kodi yanayosafirishwakupitia nchini tu, bali pia zinahakiki mafuta hayo yanakuwa hayajachakachuliwa hadi kufika katika nchi jirani za Rwanda, Burundi, DRC mashariki, Malawi na Zambia.

EWURA kwa kutumia mashine hizo zilizofungwa kwenye magari yao,inakagua vituo vya mafuta na matangi na mashine zinatoa taarifa za hali ya juu kupitia kwenye kompyuta ambayo inatoa majibu yaliyokusudiwa ambayo yanahifadhiwa pia kwa matumizi ya baadaye.

Katika kuwajali wadau, Mamlaka ilitoa kipindi cha miezi minne kwao kumaliza shehena ya mafuta isiyohusiana na upimaji wa mashine za XRF kabla ya kuanza kupima sampuli za mafuta vituoni.

Upimaji sampuli ulianza Februari 2011 na ukakamilika Aprili mwaka huo huo, ambapo vituo 235 katika mikoa 12 ya Tanzania vilikaguliwa na sampuli zikawekwa alama.

Ukaguzi huo ulibaini kuwa vituo 54 vilikuwa na mafuta yaliyochakachuliwa, ambavyo ni asilimia 23 ya vituo vyote vilivyokaguliwa. Katika ukaguzi wa kushtukiza matangi 22 yalikaguliwa katika barabara ya Dar es Salaam-Morogoro na mipakani mwa Tanzania na Rwanda hata na Burundi na Sampuli zilizochukuliwa katika matangi matatu, sawa na asilimia 14 ya matangi yote yaliyokaguliwa zilikuwa na mafuta yalikuwa yamechakachuliwa.

Waliobainika kukwepa kodi, walilipa baada ya kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA).

Kwa ujumla, matumizi ya XRF na ukaguzi endelevu, yamekuwa na ufanisi mkubwa kutokana na ushirikiano baina ya Ewura na Kampuni za Mafuta Tanzania (TAOMAC), ambazo kwa pamoja, zimeunda kamati ya watu watano ya kufuatilia na kupima utekelezaji wa mashine pamoja na kuchambua changamoto zinazojitokeza kila wiki.

Kamati hiyo imekuwa ikafanya ukaguzi wa wazi na kuhusisha wauzaji mafuta. Kaguo anasema, Ewura ipo makini katika kukagua vituo, yadi, maghala ya mafuta ya akiba na kufuatilia nyendo za wafanyabiashara wanaochakachua mafuta vituoni, hata vile vilivyoko pembeni ya barabara ya Morogoro na Mbagala-Mkuranga.

Mamlaka kwa kushirikiana na halmashauri ya mji wa Kibaha imevunja baadhi yadi za nyuma ya vituo vya mafuta zilizotumika kuchakachua, na inaendelea na ukaguzi wa vituo na matangi ili uchakachuaji uwe historia.

Ewura inakusudia kuanzisha utaratibu wa kutoa takwimu za mauzo ya mafuta kila mwezi katika kila kituo, kubainisha vituo vilivyoibuka baadaye, umbali wa kati ya vituo, na kujiridhisha kuhusu ujenzi kama umezingatia sheria na mfumo wa biashara ya mafuta.

**Changamoto**

Mamlaka inakabiliwa na changamoto ya kufanya ukaguzi mfululizo vituoni nchini, kukagua matangi yanayosafirisha mafuta hadi mipakani kwa kushirikiana na TRA na kukabiliana na udanganyifu wa vipimo vya kupimia mafuta ambavyo havioneshi kiasi cha mafuta yaliyochukuliwa.

**Matarajio**

Kaguo anasema mamlaka inakusudia kuanzisha mfumo mzuri wa ushirikiano na wauza mafuta na kuboresha taarifa zinazokusanywa na mashine ya XRF na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza na kutafuta na kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wananchi na wafanyabiashara kuhusu utandaji wa sekta hiyo kupitia vyombo vya habari.

# Juhudi za usambazaji umeme vijijini: Mwenga Hydro Limited yaonesha njia

Wateja 2,600 ambao wanaishi katika vijiji 14 katika tarafa za Ihanu, Luhunga na Mdabulo watafaidika na ruzuku hiyo kwa kuunganishiwa umeme kwa gharama nafuu.

**Na Msafiri Mtepa**



Sehemu ya bwawa litakalotumika kuzalishia umeme wa Mwenga, Mufindi.

Mwenga Hydro Limited (MHL) inatekeleza mradi wa umeme wa Megawati nne (4MW) ambao utazambazwa vijijini katika wilaya ya Mufindi, Iringa, hatua ambayo itaiwezesha kampuni hii kuuza asilimia 80 ya umeme wake kwa TANESCO kwa kutumia Mkataba wa Ununuzi wa Umeme (Standardised Power Purchase Agreement). Kiasi cha asilimia 20 kitauzwa kwa Kampuni ya Chai Mufindi ya wateja wa reja reja, kupitia Kambuni ya Rural Power Development Limited (RPDL).

MHL ni kampuni tanzu ya Mufindi Tea and Coffee Limited. Ujenzi wa mtambo wa kuzalishia umeme umefikia kiwango kinachotia moyo na inatarajiwa kwamba mnamo mwishoni mwa mwezi Juni, mtambo huo utajaribiwa. Vilevile, ujenzi wa mfumo na njia za usambazaji bado unaendelea.

Ili kuhamasisha wateja wengi kuunganishiwa umeme, MHL iliomba ruzuku toka Umoja wa Ulaya (EU) ambayo iliweza kugharamia asilimia 49.17 ya gharama zote za mradi na kupunguza kiasi kikubwa cha gharama za kuunganisha umeme kwa wateja.

Wateja 2,600 ambao wanaishi katika vijiji 14 katika tarafa za Ihanu, Luhunga na Mdabulo watafaidika na ruzuku hiyo kwa kuunganishiwa umeme kwa gharama nafuu. Pia, MHL imeomba ruzuku toka kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ili kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja wengine baada ya kukamilisha wateja 2,600 wa awamu ya kwanza

Hamu ya kupata umeme ilijionesha katika mkutano wa kukusanya maoni ulioitishwa na EWURA mnamo tarehe 18 Mei 2012, ambao ulifanyika katika ukumbi wa Igoda, kata ya Luhungo, baada ya kampuni ya MHL kutuma maombi tyake ya kuuza umeme kwa jamii husika.

Namna wanavijiji walivyoshiriki katika mkutano huu ni ushahidi tosha wa ukweli huu. Pamoja na kwamba mkutano huo ulifanyika katika muda wa kazi, ushiriki ulikuwa mzuri sana; ni kama kila mmoja alikuwa anasema "tunataka umeme sasa...mradi umechelewa sana".

Katika kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza, MHL iliahidi kuwa itawasha umeme mwanzoni mwa mwezi wa Julai baada ya kufanikiwa majaribio ya mtambo mwishoni mwa mwezi Juni, ikiwa ni kuchelewa kwa mradi kwa miezi miwili kama ilivyokuwa imepangwa hapo awali.

Tarehe hiyo ilionekana bado ni mbali kuwaridhisha wananchi pamoja na kwamba matatizo ya kijiografia na kiufundi yaliiokoa MHL ambayo ingetakiwa kutoa maelezo ya kina kuwaridhisha vinginevyo wananchi ambao wanahitaji umeme kwa muda mrefu.

Tarehe 17 Mei 2012 Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya EWURA walitembelea eneo la mradi na kuridhishwa na kiwango kilichofikliwa katika utekelezaji wa mradi. Mtambo wa kuzalishia umeme upo katika hatua za mwisho kukamilika na vilevile njia za usambazaji umeme zinaendelea kujengwa.

Umeme ni lazima, lakini si kigezo peke yake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa jamii za vijijini. Usambazaji umeme vijijini utasaidia kuamsha maendeleo endelevu na hivyo kuifanya dunia yetu ikalike kwa usalama. Ni kweli kwamba usambazaji umeme vijijini umegubikwa na changamoto za kifedha, na kampuni ya MHL inatakiwa kupongezwa kwa juhudi ilizofanya, ikiwa ni pamoja na msaada toka Umoja wa Ulaya.

Katika kusaidia juhudi za TANESCO, Sheria ya Umeme, Sura Na. 131 pamoja na Sera ya Nishati ya mwaka 2003, imefungua milango kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika kutoa huduma ya umeme hapa Tanzania. Kiwango cha kuridhisha kimefikiwa, lakini zaidi ni katika mfumo wa wazalishaji binafsi umeme (IPPs) kwa kusaini Mikataba ya Ununuzi wa Umeme na TANESCO, mikataba ambayo inatawaliwa na kanuni ya chukua au lipa. Hivyo, wawekezaji hawa wanakwepa changamoto za kutoa huduma kwa wateja wa rejareja

# Mbinga kupata umeme wa maji wa *Megawati* 7.5

Sehemu ya umeme utakaozalishwa utauzwa Tanesco chini ya mpango wa Miradi Midogo ya Umeme.

### Na Wilfred Mwakalosi

Vijiji kadhaa wilayani Mbinga huenda vikapata umeme hivi karibuni mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Taasisi ya kidini ya African Benedictine Sisters ya Mt. Agnes – Chipole.

Kwa mujibu wa maombi ya leseni yaliyotangazwa hivi karibuni na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA), African Benedictine Sisters ya Mt. Agnes inataka kuwekeza katika miundombinu ya kuzalisha umeme wa maji wa megawati 7.5 kwenye eneo la Tulila kwenye mto Ruvuma, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma.

Sehemu ya umeme utakaozalishwa utauzwa Tanesco chini ya mpango wa Miradi Midogo ya Umeme. Mradi huu wa Mbinga ni wa karibuni kabisa katika mlolongo Makubaliano mahsusi ya Ununuzi wa Umeme.

Mradi huu wa Mbinga unakuja wakati ambapo kuna mradi mwingine wa Haidrolojia wa Mwenga—Mwenga Hydro Limited—ambao umeanza kazi hivi karibuni, kwa kufua megawati nne kwa ajili ya umeme vijijini huko wilaya ya Mufindi, ambapo kampuni hiyo itaiuzia Tanesco takriban asilimia 80 ya umeme huo. Umeme unaobaki kitauziwa kiwanda cha chai cha Mufindi na wateja wa reja reja, kupitia mpango wa umeme vijijini.

Mradi huu wa Mbinga licha ya kuiuzia Tanesco umeme, utasambaza sehemu nyingine ya umeme huo kwenye vijiji vya Mpepai, Mipeta, Kihungu, Mapendano na Pacha Sita.

Vijiji vingine vitakavyofaidika na umeme huo ni Kizuka, Magagura, Masangu, Nakahegwa, Matomondo, Mbinga Mwalule, JKT-Mlale na Chuo Cha Maendeleo ya Jamii-Mlale, ambavyo viko jirani na mradi.

Umuhimu wa nishati ya umeme ni mkubwa lakini nishati hiyo imekuwa haitoshelezi mahitaji ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwenye jamii za vijijini. Kupatinakana kwa umeme kwa namna hii kutasababisha maendeleo yatayoifanya dunia iwe sehemu bora zaidi ya kuishi.



**Hali mbaya ya hewa iliyosababisha upungufu wa maji kama inavyooneka kwenye sehemu ya bwawa hili la Mtera, inailazimu sekta ya nishati kushirikiana na sekta binafsi katika kuwekeza zaidi kwenye miundo mbinu ya uzalishaji umeme ili kukidhi mahitaji ya umeme ya taifa.**

# Our Areas of Regulation

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority



Petroleum Products



Natural Gas



Emergency Measures against Power Shortage



Electricity



Sewarage



Water

**Our Vision:**
Quality, affordable and sustainable energy and water services for all

**Our Mission:**
To champion the delivery of energy and water services through world-class regulation for enhencement of the welfare of the Tanzanian society

**Our Core Values**

a) Transparency
b) Intergrity
c) Responsiveness
d) Diligence
e) Accountability
f) Courtesy
g) Honest
h) Excellence
i) Equity and
j) Professionalism

**For Information Contact:**

Energy and Water Utilities Regulatory Authority
6th Floor, Harbour View Towers,
Samora Avenue / Mission Street
P.O. Box 721775, Dar es Salaam,
**Tanzania**
Tel: +255 (0) 22 212 3850/3/4,
Fax: +255 (0)22 212 3180

**email: info@ewura.go.tz**
**website: www.ewura.go.tz**

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Mkurugenzi wa EWURA wa Udhibiti wa Uchumi Bw. Felix Ngamlagosi (Kushoto) na Mkurugenzi mwenzake wa Umeme, Mhandisi Anastas Mbawala, (wa pili kulia), wakitembelea bwawa la kuzalishia umeme la Kidatu pamoja na maofisa wa Tanesco tarehe 14, Septemba 2012.**



**Mkurugenzi wa EWURA wa Udhibiti wa Uchumi Bw. Felix Ngamlagosi (Kulia) na Mkurugenzi wa Umeme, Mhandisi Anastas Mbawala, (wa pili kulia), wakijadili jambo na maofisa wa Tanesco walipotembelea Kituo cha kuzalisha umeme cha Kidatu, tarehe 14, Septemba 2012.**

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Mkuu wa Mkoa wa Singida, Parseko Ole Kone (mwenye suti) akiuliza swali wakati wa maelezo mafupi yaliyotolewa na Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA Bw. Titus Kaguo, (mwenye fulana nyeupe) kuhusu namna mtambo maalum wa kupimia mafuta wa XRF unavyoweza kubaini mafuta machafu, kwenye maonesho ya Nane Nane, Dodoma Agosti 2012. Kulia ni Mkaguzi Mkuu wa EWURA wa Bidhaa za Petroli Mhandisi. Julius Gashaza.**




**Mkuu wa Mkoa wa Singida, Parseko Ole Kone (mwenye suti) akihojiwa na Mwandishi wa habari Bw. Paschal Mayala mara baada ya kutembelea banda la EWURA wakati wa maonesho ya Nane Nane mjini Dodoma, Agosti 2012.**

# MATUKIO KATIKA PICHA




**Elimu kwa Umma: Baadhi ya watu waliotembelea banda la EWURA wakisikiliza maelezo kuhusu maabara ya XRF inavyofanya kazi, wakati wa maonesho ya Nane Nane, Dodoma, Agosti 2012.**



**Sehemu ya bwawa la Kidatu likionekana kuwa na kina kidogo cha maji, jambo ambalo limeathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa umeme. Picha hii ilipigwa Septemba 14, 2012.**

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Baadhi ya wajumbe wa bodi ya EWURA wakipata maelekezo toka kwa Afisa wa Mwenga walipotembelea maporomoko ya kuzalishia umeme ya Mwenga, huko Mufindi, Mkoani Iringa hivi karibuni.**



**Mkurugenzi wa EWURA wa Udhibiti wa Uchumi, Bw. Felix Ngamlagosi (Kulia), akitazama mtambo wa kuzalishia umeme Kihansi, huku Meneja wa kituo hicho Mhandisi Pakaya Mtamakaya akimwangalia.**

# ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

## EWURA regulates: **Electricity, Petroleum, Gas and Water Services**









**Our Vision**
Quality, affordable and sustainable energy and water services for all.

**Our Mission**
To champion the delivery of energy and water services through world-class regulation for the enhancement of the welfare of the Tanzanian society.

**Our Duties**
- Promoting effective competition and economic efficiency
- Protecting the interests of consumers
- Protecting the financial viability of efficient suppliers
- Promoting the availability of regulated services to all consumers including low income, rural and disadvantaged consumers
- Taking into account the need to protect and preserve the environment when performing its functions
- Enhancing public knowledge, awareness and understanding of the regulated sectors including rights and obligations of consumers and regulated suppliers, ways in which complaints and disputes may be initiated and resolved and the duties, functions and activities of the Authority.
-
- **Our Functions**
- Issue, renew and cancel licences
- Initiating establishment of standards for goods and services
- Establish standards for terms and conditions of supply of goods and services
- Regulate rates and charges
- Make rules
- Monitor the performance of regulated sectors in relations to levels of investment, availability quality and standards of services, cost of services and efficiency of production and distribution of services.
- Facilitate the resolution of complaints and disputes.

6th Floor, Harbour View Towers, Samora Avenue, P.O. Box 72175, Dar es Salaam, Tanzania
**Tel:** +255 22 212 3850/3/4/6, **Fax:** +255 22 212 3180 / 21324778

Email: info@ewura.go.tz Website:www.ewura.go.tz